



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU CHANJO YA POLIO AWAMU YA NNE KWA WATOTO WENYE UMRI WA MIAKA 0 - 5

Mwanhuzi, Tarehe 30 Novemba 2022.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, Msoleni Dakawa anapenda kuutaarifu umma kuwa Halmashauri itanza rasmi zoezi la Kitaifa la kutoa **CHANJO DHIDI YA UGONJWA WA POLIO** kwa watoto wa kuanzia **miaka 0 – 5** ambalo litafanyika kwa siku nne yaani kuanzia **tarehe 01 – 04 Desemba 2022.**

Dakawa amesema Chanjo hiyo ya matone itatolewa kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya Serikali na vya binafsi ambavyo vitafunguliwa kuanzia saa **02:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.**

Aidha, Mkurugenzi Dakawa amebainisha kuwa kutakuwa na huduma **maalum ya Mkoba (Mobile Clinick)** kwenye maeneo ambayo yapo mbali na vituo vya kutolea huduma za afya na baadhi ya maeneo chanjo hiyo itatolewa kwenye Ofisi za Vijiji/Kata kwa kuzingatia taratibu zilivyopangwa na Divisheni ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe.

Hivyo, Wazazi/walezi wote wenye watoto wa umri huo mnatakiwa kuwapeleka watoto kupata chanjo hiyo muhimu kwenye vituo vilivyopo karibu na maeneo wanayoishi ili kuwakinga dhidi ya ugonjwa huo wa kupooza kwani ni hatari na unasababisha udumavu na ulemavu wa viungo kwa watoto.

'KINGA NI BORA KULIKO TIBA'

Benton J. Nollo

MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI